# Nyaraka za awali za mipango ya huduma zinazotolewa Queensland

### Mwongozo wa awali wa Huduma ya Afya (Advance Health Directive)

Huu ni waraka wa kisheria unaoelezea maamuzi yako na unaoongoza huduma yako ya afya ya baadaye katika mazingira maalumu wakati ambapo unaweza usiweze kufanya maamuzi na kuwasiliana. Ni lazima isainiwe na daktari wako, mwakilishi wa kisheria na kushuhudiwa. Fomu zinapatikana kupitia **justice.qld.gov.au**.

### Nguvu ya kudumu ya Wakili (Enduring Power of Attorney)

Huu ni waraka unaomteua mtu au watu wa chaguo lako kufanya maamuzi muhimu kwa niaba yako unapokuwa hauna uwezo wa kufanya hivyo wewe mwenyewe. Ni sharti isainiwe na mwakilishi wa kisheria Pamoja na mtu wa chaguo lako. Fomu zinapatikana kupitia **justice.qld.gov.au** ama ongea na wakili wako au Mdhamini wa uma

### Tamko la Chaguo (Statement of Choices)

Waraka huu unazingatia utashi wako, maadili na Imani. Unaweza kuwasaidia watu wako wa karibu kufanya maamuzi ya kiafya kwa niaba yako, kama yakihitajika. Unatoa faraja kwako na wapendwa wako. Ni lazima isainiwe na daktari. Fomu zinapatikana kupitia my**care**my**choices**.com.au, ongea na daktarin wako au wasiliana na Ofisi ya Mipango ya Huduma ya Awali.

### Ofisi ya Mipango ya Huduma ya Awali

Ofisi ya Mipango ya Huduma ya Awali, Huduma za afya Queensland, ni huduma ya bure na ya faragha kwa watu wote wa Queensland kuwasaidia katika mchakato wa maandalizi ya huduma ya awali, inayojumuisha,

- Kutoa fomu na vifurushi vya taarifa za mipango ya huduma ya awali
- Kukushauri ni nani wa kuongea naye kuhusu mipango ya huduma ya awali katika eneo lako
- Kuongeza nakala za nyaraka za huduma yako ya awali kwenye kumbukumbu za huduma yako ya afya za Queensland
- Kujibu maswali yako yote kuhusu mipango ya huduma ya awali

### Wasiliana na Ofisi ya Mipango ya Huduma ya Awali


1300 007 227

1300 008 227

PO Box 2274, Runcorn Qld 4113

acp@health.qld.gov.au

my**care**my**choices**.com.au


Huduma ya ufasili inapatikana wakati wa masaa ya kazi kutoa taarifa na rasilimali kuhusu mipango ya huduma ya awali ya Queensland

**Piga simu 13 14 50**

Interpreter

- Taja lugha unayoongea
- Omba kuunganishwa na ofisi ya Mipango ya huduma ya awali kupitia **1300 007 227**.

# Huduma yangu Chaguo langu

Swahili

Kama ulijeruhiwa kwa ghafla ama ulikuwa mahututi, ni namna gani wahudumu wa afya watajua mahitaji yako ya huduma ya afya



*Jiwezeshe kujipanga kwa huduma yako ya afya ya baadaye*

my**care**my**choices**.com.au

OACP
Statewide Office of Advance Care Planning

Queensland Government

# Nini maana ya Mipango ya Huduma ya Awali?

Mpango wa huduma ya awali ni mchakato wa kufikiria na kuwasiliana kuhusu mahitaji yako ya huduma ya afya ya baadaye. Mipango ya huduma ya awali inatumika katika mazingira unapokuwa huwezi kuongea mwenyewe.

Mipango ya huduma ya awali ni ya makusudi na inaweza kujumuisha:

- Kufikiria na kujadiriana kuhusu maadili yako, aina tofautitofauti za huduma ya afya unazopendelea na ubora wa chaguo lako la maisha na watu unaowamini.
- Kumchagua mtu mmoja, au zaidi, mbadala wa wafanya maamuzi kwa niaba yako, kama watahitajika
- Kuandika mahitaji yako ya huduma ya afya katika kumbukumbu

Kama vile kufanya wosia, mpango wa huduma ya awali inahusu kupanga kwa ajili ya Maisha yako ya baadaye

# Kwa nini kupanga mapema?

Mpango wa huduma wa awali unawezesha:

- Matibabu na huduma unayoipata huzingatia utashi wako
- Wapendwa wako wanajua unachohitaji kama watatakiwa kufanya maamuzi kwa niaba yako
- Maamuzi ya huduma za afya hayafanywi tu tatizo linapojitokeza

# Tayari kuanza kupanga?

## Hatua ya 1-Kujadiriana

Inaweza kuwa vigumu kuongelea kuhusu nini unaweza kuhitaji kama ukiwa mahututi, ila inaweza kukupa, na wale unaowapenda, utulivu wa akili kama wakijua matashi yako.

Baada ya kufikiria kuhusu mahitaji yako ya baadaye ya huduma ya afya:

- Jadiriana juu ya hali zako ya kitabibu na daktari wako na jinsi zinavyoweza kukuathiri siku zijazo
- Ongelea kuhusu mahitaji yako ya huduma za afya na familia yako na wote walio karibu yako.
- Mwombe mtu/watu unaowaamini kuwa wafanya maamuzi mbadala kwa niaba yako, kuafanya maamuzi kwa niaba yako, kama itahitajika.

## Hatua ya 2-Kumbukumbu

Tunza kumbukumbu za mahitaji na maamuzi yako kwa kukamilisha mojawapo ama zaidi ya nyaraka zifuatazo:

- Mwongozo wa awali wa Afya
- Mamlaka ya mwanasheria
- Tamko la chaguo lako

Pakua fomu hizi bila gharama kutoka: mycaremychoices.com.au

## Hatua ya 3-Shirikisha

Hakikisha matashi yako ya huduma ya afya yaliyo katika kumbukumbu yanafahamika na yanapatikana kwa wote wanaokuhudumia

Kushirikisha matashi yako:

- Toa nakala za nyaraka zako kwa wale unaowaamini (mfano wanafamilia, marafiki wa karibu, kwa mbadala wa wafanya maamuzi na watoa huduma wako wa afya (mfano daktarin)

**NA**

- Toa nakala ya nyaraka zako kwenye Ofisi ya Mipango ya Huduma za awali zinazotakiwa kuongezwa kwenye kumbukumbu ya Huduma zako za afya za Queensland (**tazama juu kwa chaguzi**)
- Pandisha nyaraka zako kwenye "My Heath Record" kupitia **myhealthrecord.gov.au**

## Hatua ya 4-Hakiki

Ni muhimu kuhakiki nyaraka zako ya Mipango ya huduma za awali kila mara, hasa kama hali afya yako inabadirika au kama ukibadirisha mahitaji yako ya huduma za afya.

